**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HUTUBA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAJUMUISHO YA MJADALA WA BAJETI ZA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kuendelea kutukarimu neema ya uhai na afya njema sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na pia kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa hali ya amani na utulivu. Aidha, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wawili wa Baraza kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yenu ya kutuongoza katika Baraza wakati tukiendelea kutekeleza wajibu wetu wa kikatiba wa kuidhinisha bajeti kwa niaba ya wananchi wetu ambao tunawawakilisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa moyo wa dhati napenda kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uongozi wake mahiri ambao kwa muda mfupi umewajengea imani na matumaini makubwa wananchi wa Zanzibar katika harakati za kujikomboa na umasikini, kujenga jamii yenye umoja na mshikamano pamoja na kuiletea maendeleo na ustawi nchi yetu ya Zanzibar. Aidha, niwapongeze pia wasaidizi wake wa karibu Makamo

wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdullah kwa namna wanavyojitolea kwa moyo wao wote katika kumsaidia Mhe. Rais katika kufanikisha malengo ya nchi yetu tuliyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,** Shukurani maalum naomba nizipeleke kwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti inayoundwa na Wajumbe mahiri ambao nakiri kwamba wamenipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu. Ili kuzipa nguvu shukurani zangu kwao naomba uniruhusu niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo;-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Anna Athanas Paul | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Harusi Said Suleiman | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraji Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |

Aidha, napenda pia kuwashukuru makatibu wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano wao na uratibu wa shughuli za Kamati, naomba pia kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Abdalla Ali Shauri | Katibu |
| 2. | Ndg. Asha Said Mohammed | Katibu |
| 3. | Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| 4. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,** Hutuba hii ya majumuisho ya mjadala wa Bajeti inatokana na maelekezo ya Kanuni ya 101(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2020 ambayo inaelekeza Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti kufanya majumuisho kwa kuzingatia hoja zilizoibuka wakati wa mjadala wa Bajeti za Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba niliarifu Baraza lako kuwa, Kamati yangu imepata fursa ya kukaa na Serikali na kujadiliana kuhusu Hoja za kibajeti hususan hoja ambazo hazikupatiwa ufafanuzi wa kutosha na ambazo pia ulielekeza zikajadiliwe katika Kamati ya Bajeti kwa lengo la kupatiwa ufafanuzi wa ziada ambao ulikosekana wakati wa kupitisha mafungu ili majibu yake yawasilishwe Barazani. Hivyo, hutuba hii ni majibu ya mashauriano ya kikao hicho kwa hoja zilizojadiliwa pamoja na maoni ya Kamati kutokana na majibu ya Serikali yaliyotolewa.

## UFANUZI WA HOJA ZILIZOJADILIWA WAKATI WA KIKAO CHA MAJUMUISHO BAINA YA SERIKALI NA KAMATI YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa kikao cha majumuisho baina ya Kamati na Serikali jumla ya Hoja nane (8) kutoka katika Wizara tofauti zilijadiliwa. Wizara ambazo Hoja zao zilijadiliwa ni kama ifuatavyo:

1. Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala bora
2. Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto
3. Wizara ya Maji, Nishati na Madini
4. Wizara Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo
5. Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo
6. Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

**Mheshimiwa Spika**, ili kutowa urahisi wa ufafanuzi wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati, Kamati yangu imeziweka hoja hizo katika mfumo wa Jadweli ambalo limegawika Sehemu Nne; Sehemu ya Kwanza inahusu Hoja zilizoibuliwa, Sehemu ya Pili inahusu Majibu ya Wizara na Sehemu ya Tatu ni Ushauri wa Kamati ya Bajeti.

| WIZARA YA NCHI, AFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA | | | |
|---|---|---|---|
| SNo. | HOJA | MAJIBU YA WIZARA | MAONI YA KAMATI |
| 1. | Katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ya mwaka 2020/2021, Fungu G04 (Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka) lilipangiwa na kuidhinishiwa jumla ya TZS 3,754,700,000. Aidha, katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2021/2022, imeelezwa kwamba Fungu hili limepangiwa jumla ya TZS 2,293,912,500 (**Ukurasa 38**). Aidha katika Kitabu cha Makadirio ya Bajeti (**Ukurasa G04-6**), jumla kuu ya Fungu G04 kwa mwaka 2020/2021 ni TZS 3,754,700,000. Hoja ya Kamati ni kuwepo kwa tofauti ya fedha katika Fungu hili. | Wizara walikiri utofauti wa Fungu G04 (Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka) baina ya kitabu cha Hutuba Waziri kwa mwaka 2021/2022 na Kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/2022. Takwimu iliyo sahihi ni ile iliyopo katika kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/2022 TZS 3,754,700,000. Upungufu wa fedha ambazo hazikuripotiwa katika kitabu cha Hotuba zilikuwa ni fedha za ruzuku katika Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti na fedha za miradi ya maendeleo. | Kamati ilipotia Vitabu vya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa 2021/2022 na 2020/2021 pamoja na Sheria ya Matumizi ya mwaka 2020/2021 imebaini kwamba fedha zilizotengwa kwa Fungu G04 kwa mwaka 2020/2021 ni TZS 3,754,700,000. Hivyo, kasoro hizi haziathiri bajeti lakini Wizara zinapaswa kuwa makini ili kuondosha mkanganyiko. |

| WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO | | | |
|---|---|---|---|
| SNo. | HOJA | MAJIBU YA WIZARA | MAONI YA KAMATI |
| 1. | Kamati ilitaka kujua idadi ya wazee waliosajiliwa katika Pencheni Jamii kwa mwaka 2020/2021 na kiasi cha fedha walizolipwa kutokana na kuwepo kwa utofauti wa kitakwimu kati ya wazee waliyolipwa mwaka 2019/2020 na 2020/2021 na kiasi cha fedha walicholipwa. Aidha, Kamati ilipata wasiwasi wa ubadhirifu wa fedha za umma katika ulipaji wa pencheni hii. | Wizara ilikiri takwimu zilizopo katika Kitabu cha Hotuba ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 si sahihi na Kamati ilipatiwa takwimu sahihi zilizoonesha idadi wa wazee waliostahiki kulipwa ambayo ni 28970, Unguja 17898 na Pemba 11072. Aidha, Jumla ya fedha zilizolipwa kwa bajeti ya 2020/2021 hadi kufikia Machi ni TZS 5,430,532,630. | Kamati inasisitiza Wizara kuwa makini katika kuandaa takwimu zinazohusiana na taarifa za bajeti tatizo ambalo pia limejitokeza kwa Wizara nyengine mbali mbali. Kutokuwa na takwimu sahihi kunapelekea kutokuwa na ufanisi wa matumizi wa fedha za umma lakini pia hatutokuwa na mipango inayoakisi uhalisia. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Kamati ilitaka kujua ni kampuni gani inayofanya usafi na gharama zake. Wakati wa mjadala wa bajeti hoja hii haikupata ufafanuzi kwani Waziri aliomba kupatiwa muda wa kuifanyia kazi kwa kupata muda wa kupitia mikataba husika. | Kamati iliarifiwa kuwa kampuni inayofanya usafi kwa Hospitali ya Mnazi mmoja na Mwembeladu ni Kampuni ya Astonish na gharama yake ni TZS 231,690,064 kwa mwaka. | Kwa kuwa Wizara ina watumishi maalum (orderly) ambao wameajiriwa kwa ajili ya kufanya shughuli za usafi, Kamati inaishauri Wizara kuwatumia watumishi hao kwa ajili ya usafi ili kupunguza gharama za usafi. Aidha, usafi wa hospitali unahitaji watendaji wenye ujuzi maalum. |
| **WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI** | | | |
| **SNo.** | **HOJA** | **MAJIBU YA WIZARA** | **MAONI YA KAMATI** |
| 1. | Katika mwaka 2020/2021, fedha za ruzuku ya mishahara zilizopatikana zilikuwa TZS 2.7 bilioni, kiasi hichi hakitoshelezi kulipa mishahara na fedha iliyobaki inapaswa kulipwa na Mamlaka ya Maji (ZAWA) kutoka katika vyanzo vyake na ukiangalia mapato ambayo ZAWA wamepata hayatoshelezi kulipa kiasi kilichobaki, Kamati iliomba ufafanuzi katika jambo hili. | Kamati imearifiwa kwamba ZAWA, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 wamepata ruzuku ya mshahara ya jumla ya TZS Bilioni 2.7 kwa kipindi cha miezi tisa na ZAWA wamekiri mbele ya Kamati kiwango cha mshahara kilichobaki baada ya kupata ruzuku wataweza kukilipa. | Kamati imeridhishwa na ufafanuzi uliotolewa. Aidha, kutokana na changamoto ya upatikanaji wa maji katika maeneo tofauti, Kamati inashauri Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyopangwa kwa bajeti ya 2021/2022 zinapatikana kwa wakati. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Katika miradi ya maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ambayo imeelezwa katika program ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji kumepatikana TZS 22.438 bilioni (Kiambanisho nambari 1. Ukurasa wa 41 kitabu cha ya Hotuba ya Waziri). Kati ya fedha hizo, TZS 525.393 milioni ni kutoka SMZ na TZS 21.912 bilioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, kwa mujibu wa Waziri, fedha zilizopatikana kutoka SMZ kwa ajili ya Mradi wa Visima vya Ras el Khemah tu ni TZS 1.3 bilioni. Kamati iliomba ufafanuzi zaidi na Waziri aliahidi kutoa taarifa za ziada ili kuondoa mkanganyiko. | Wizara imethibitisha kwamba, fedha zilizopatikana kutoka SMZ kwa ajili ya Mradi wa visima vya Ras alkhaima ni TZS 1.3 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 525.393 milioni zilizoripotiwa awali na 773,000,000 hazikuripotiwa awali kwasababu ziliingia mwisho mwa mwezi wa Machi, 2021. | Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kushirikiaana na Wizara ya Maji, Nishati na Maadini kuweka sawa taarifa za fedha za Mradi huu ili kuondosha utata uliyojitokeza. |

| WIZARA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO | | | |
|---|---|---|---|
| SN | HOJA | MAJIBU YA WIZARA | MAONI YA KAMATI |
| 1. | Hoja ya Kamati ni kuhusu uhalali wa matumizi ya TZS 1,147,696,900 ambayo yametumika katika mradi wa ujenzi wa ofisi na studio za ZBC PEMBA. Kamati imetaka kujua fedha hizi zilizotumika zimetoka katika kasma gani wakati kasma iliyopangiwa ya mradi huu katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 haijaoneshwa katika Bajeti ya 2020/2021. | Kamati imearifiwa kuwa matumizi ya TZS 1,147,696,900 ambayo yametumika katika mradi wa ujenzi wa ofisi na studio za ZBC PEMBA yametoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali. | Kamati inaishauri Afisi ya Rais Fedha na Mipango, iwapo itatumia fedha za Mfuko Mkuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo fedha zipelekwe moja kwa moja kwa mkandarasi badala ya kupitia kwa Wizara na Afisi ya Rais Fedha na Mipango inapaswa kuripoti taarifa za utekelezaji wa mradi kwa kuzingatia kuwa wao ndio waliodhinishiwa fedha hizo. |

| WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO | | | |
|---|---|---|---|
| | HOJA | MAJIBU YA WIZARA | MAONI YA KAMATI |
| 1. | Ufafanuzi katika kifungu PL 0202 Programu Kuu ya Mendeleo ya Uvuvi ambapo shughuli zinazohusiana na uvuvi kujitokeza katika Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na pia fungu linalohusiana na uvuvi kujitokeza tena katika Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo. | Kamati imearifiwa kwamba kujitokeza kwa Programu Kuu ya Mendeleo ya Uvuvi kwa Wizara mbili tofauti kunatokana na kwamba, shughuli za uvuvi awali zilikuwa zinaratibiwa na Wizara ya Kilimo na ambapo kwa sasa shughuli hizo zimehamishiwa katika wizara ya Uchumi wa Buluu na hakuna athari yoyote kwani program ya Maendeleo ya Uvuvi katika Wizara ya Kilimo imeripotiwa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/2021 na kwa bajeti 2021/2022 ya program hiyo imeidhinishwa katika wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. | Kamati imeridhika na ufafanuzi uliotolewa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Kuhusu Fungu **PL0101** maendeleo ya kilimo na **Fungu PL0103** maendeleo ya mifugo. Hoja ya Mjumbe ni kutaka kupata ufafanuzi kuhusiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo **(ZALIRI),** Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar **(ZARI)** na Taasisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, kuwa taasisi hizi zimeomba kuidhinishiwa ruzuku katika taasisi ambazo zinapokea OC wakati taasisi hizi kwa mwaka fedha 2021/2022 zimefanywa kuwa huduma. | Wizara imekiri mbele ya Kamati kuwa, taasisi hizi zinapokea ruzuku lakini ruzuku hiyo inatoka katika OC ya Wizara. | Kamati imeshauri Wizara kwa Taasisi ambazo zinajitegemea pia zipangiwe program zake badala ya kuwekwa kama ni huduma chini ya program za Idara nyengine ili kuondoa mkanganyiko wa kiutendaji na uwajibikaji. |

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine Hotuba hii imezingatia maeneo ambayo yalichangiwa na wajumbe wengi na hoja za jumla zilizojitokeza katika mjadala wa Bajeti kwa mwaka 2021/2022.

## MAENEO AMBAYO YALICHANGIWA NA WAJUMBE WENGI

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa mjadala wa Bajeti, Waheshimiwa Wajumbe walichangia katika maeneo mengi yaliyohusu sekta tofauti. Hata hivyo, kuna maeneo mahsusi ambayo yalibahatika kuchangiwa na Wajumbe wengi zaidi na baadhi ya maeneo yalichangiwa kwa hisia kubwa. Mheshimiwa Spika, kwakuwa hii ni hutuba ya majumuisho ni vyema Kamati yangu ikayakumbushia maeneo hayo japo kwa uchache wake kwa lengo la kuikumbusha Serikali kuyachukulia uzito maalum maeneo hayo na kuyafanyia kazi. Maeneo haya ni kama yafuatayo:

### Wizara ya Nchi, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Mijadala ya wajumbe imeonesha kuwa, Miradi inayohusiana na mazingira haijatekelezwa katika kiwango kizuri ikiwemo Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi. Hivyo Kamati inaungana na wajumbe katika kusisitiza utekelezaji wa miradi hiyo katika kiwango kinachostahiki pamoja na kuitaka Serikali kuhakikisha inachangia vyema miradi hiyo kwa Bajeti ya 2021/2022 kwani katika utekelezaji wa Bajeti ya 2020/2021 hadi kufikia Machi, 2021 hakukuwa na fedha ya mchango wa Serikali iliyopatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe walichangia juu ya utumiaji wa madawa ya kulevya katika maeneo mbali mbali na namna Serikali inavyobeba mzigo wa

kuhudumia watumiaji hao ambao asilimia kubwa ni vijana na ndio tegemeo kubwa katika uzalishaji. Katika kukabiliana na hali hii, Kamati inasisitiza mashirikiano ya pamoja baina ya Serikali, taasisi mbali mbali na wananchi katika kuchukua hatua za kupinga utumiaji wa madawa hayo.

### Wizara ya Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wajumbe wengi walisisitiza kuhusu fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi na kuwafikia kama ilivyokusudiwa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhusu fedha hizo ili kubaini mafanikio na kasoro zinazojitokeza.

### Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uchache wa fedha za bajeti zinazotengwa katika kuutangaza utalii na kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya utalii katika uchumi wetu, ni vyema Serikali katika upangaji wa bajeti zijazo ikafikiria namna ya kuongeza fedha za kuutangaza utalii badala ya kupunguza kama ilivyojitokeza katika bajeti hii ya 2021/2022. Aidha, Serikali inapaswa kushirikiana kwa ukaribu na wadau mbali mbali wa sekta ya utalii katika kuutangaza ndani na nje ya nchi.

### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya kuwa, kila mwaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali huidhinishiwa bajeti yao, bado wajumbe wengi walichangia changamoto ya stahiki za walimu ikiwemo maposho na madeni mbali mbali kutolipwa kwa muda unaostahiki. Kamati inapendekeza kuandaliwa mkakati

maalum wa kuondosha changamoto hii kwa kuwapatia walimu stahiki zao kwa wakati ili waweze kutekeza majukumu yao kwa ufanisi. Ni wazi kwamba, kuwepo kwa malalamiko mengi ya stahiki za walimu ina maana kwamba lipo tatizo kubwa linalohitaji kufanyiwa kazi.

**Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum**

**Mheshimiwa Spika,** eneo jengine ambalo wajumbe walichangia kwa msisitizo ni kuviwezesha vikosi vya SMZ hususan JKU na Chuo cha Mafunzo ili viweze kujitegemea. Wakati wa amani, vikosi vyetu vinapaswa kuwa wazalishaji kupitia miradi mbali mbali itakayobuniwa badala ya kuwa tegemezi kwa Serikali. Kuimarisha vikosi hivi, kutasaidia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi, kilimo, ufugaji na uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** suala la kupambana na wizi wa mazao na mifugo pia lilichangiwa kwa msisitizo mkubwa na wajumbe wa Baraza lako. Jambo hili linahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka kwani linawarudisha nyuma wananchi kiuchumi kwa kukata tamaa ya kuendelea kufanya shughuli za kilimo na mifugo. Hali hii ikiendelea, itaathiri uchumi wetu kwa kiasi kikubwa kwa sekta ya kilimo na ufugaji na kupelekea kukosekana kwa mchango wa sekta hizo katika Pato la Taifa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi**

**Mheshimiwa Spika,** jambo jengine ambalo limesisitizwa sana katika Mkutano huu wa Bajeti ni kuwepo kwa madai ya wananchi kutolipwa fidia za kubomolewa nyumba zao au vipando vya pale miradi ya barabara inapotekelezwa licha ya Serikali kukiri kwamba fedha hizo zimeshalipwa. Katika hili, Serikali inapaswa kuchukua tahadhari kubwa kwani kuna

wasiwasi kwamba fedha zimeshatolewa na Serikali lakini hazijawafikia walengwa. Kuchelewa kuwalipa wahusika, ni kuwarudisha nyuma kiuchumi na kijamii na pia kupelekea kupoteza imani na Serikali yao.

**Mheshimiwa Spika,** eneo jengine ni kutotekelezwa kwa wakati miradi ya ujenzi wa barabara za Chake Chake – Wete na Chake Chake – Mkoani na barabara za ndani  licha kupangwa katika bajeti za miaka iliyopita na nyengine kuwa na ahadi za viongozi wakuu. Hali hii ya kuwepo miradi mingi katika bajeti zetu bila ya kutekelezwa ni dalili kwamba bajeti zetu hazina uhalisia. Tunapanga mambo mengi lakini tunatekeleza kidogo tena bila ya kukamilika.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto**

**Mheshimiwa Spika,** katika Wizara ya Afya jambo ambalo limechukua muda mkubwa wa wajumbe wako kulijadili ni kutotekelezwa kwa miradi iliyopangwa. Mathalan,  Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mradi wa Upanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja,  Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wete na Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni. Miradi hii imekuwa ikitajwa kwa muda mrefu mpaka inapoteza hamu hata kuitaja. Ni muhimu sana kupanga miradi tunayohisi tutaweza kuitekeleza kulingana na hali yetu ya kiuchumi. **Mheshimiwa Spika,** ubora wa bajeti haupimwi kwa wingi wa miradi inayopangwa bali hupimwa kwa utekelezaji wake pamoja na tija itakayopatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Pia kulizungumzwa tatizo la kuingia kwa bidhaa zisizofaa kwa matumizi Zanzibar. Jambo hili lilitolewa ufafanuzi unaoridhisha, hata hivyo ipo haja ya hatua zote zilizotajwa kutekelezwa kwa haraka sana na kwa ufanisi wa hali ya juu kwani bidhaa zisizofaa kwa

matumizi hasa za chakula zinasababisha madhara makubwa ya kiafya kwa watumiaji. Hali hii inaathiri uchumi wetu kwa kupoteza nguvu kazi na kuingizia Serikali gharama kubwa za matibabu.

### Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

**Mheshimiwa Spika,** Msisitizo umewekwa pia kwa wadaiwa sugu waliopanga katika nyumba za Shirika la Nyumba Zanzibar. Jambo hili ni sawa na kuliyumbisha Shirika kwani ndio chanzo pekee cha mapato ya Shirika. Muarubaini wa hili, ni kutekeleza Sheria ya Shirika la Nyumba kwa kuwachukulia hatua bila muhali wale wote wanaodaiwa kwa muda mrefu kwani wengi wao wana uwezo wa kufanya hivyo lakini wameamua kulidharau Shirika kwani wapanganyaji wengine na wao wamewapangisha watu wengine, kitu ambacho ni kinyume cha Sheria lakini kumekuwa na ukakasi wa kulisimamia suali hili.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo jengine ni kuwepo migogoro mingi ya ardhi. Hali hii ina athari kubwa kiuchumi kwani kuna utitiri mkubwa wa kesi mahkamani ambazo zinapoteza muda mkubwa kwa wananchi kushughulikia kesi hizo, kiasi ambacho kunapelekea kukosekana kwa muda wa kufanya shughuli za kimaendeleo lakini pia inapotokezea kudhulumiwa mwenye haki kunapelekea kumrudisha nyuma kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kutofanyiwa kazi Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Zanzibar (Zanzibar Land Use Master Plan) ni miongoni mwa maeneo yaliyojadiliwa na wajumbe wengi. Hali hii imesababisha kuwepo uvamizi wa ardhi kama vile maeneo ya kilimo kujengwa nyumba za makaazi na pia kutokuwa na miji iliyopangika. Kutekelezwa kwa mpango huu, kungelitatua matatizo mengi ya ardhi kama vile migogoro ya ardhi nakadhaalika.

**Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo limechangiwa sana na wajumbe ni katika maeneo ya uwekezaji kama vile eneo la uwekezaji Micheweni Pemba ambalo hadi sasa halijawekewa miundombinu ya barabara, maji na umeme. Serikali ya awamu ya nane imeazimia kukifanya Kisiwa cha Pemba kuwa Eneo Maalum la Uwekezaji (Strategic Investment Area) kwa kuweka vivutio mahsusi kwa wawekezaji ili maendeleo ya Pemba yaende sambamba na maendeleo ya Unguja. Kamati inashauri Serikali kuharakisha upelekaji wa miundombinu katika maeneo hayo ili azma hiyo iweze kutekelezeka. Aidha, Serikali inapaswa kuharakisha kuendeleza eneo hilo ili kudhibiti uvamizi katika maeneo hayo kwani yakiwa wazi kwa muda mrefu huenda yakavamiwa na wananchi kwa kuweka makaazi na kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Hali hii, inaweza baadae ikasababisha migogoro baina ya Serikali na wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kuwawezesha wajasiriamali kitaaluma na kuwapa mikopo ni eneo jengine ambalo limechangiwa sana na Wajumbe. Kimsingi elimu ya ujasiriamali, elimu ya kuongeza thamani bidhaa na elimu ya jinsi ya kutunza mitaji ni jambo la msingi katika kuinua biashara zao na kuzifanya ziwe na tija na kuweza kuongeza kipato pamoja na kuwaongezea mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza mitaji katika biashara zao. Kufanya hivyo kutawasaidia wananchi kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea ajira kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe pia wamechangia kuhusu mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kuendeleza miradi mbalimbali ya kuichumi ili iweze kuleta tija kwa wananchi. Kamati inasisitiza umuhimu wa

mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ili kuifungua Zanzibar kiuchumi na kujiletea maendeleo ya haraka, kwani hali halisi inaonesha muitikio wa mashirikiano hayo bado ni mdogo sana, kamati inaishauri Serikali kupitia tena sera na sheria ya (PPP) ili kubaini changamoto zinazokwaza utekelezaji wake ili changamoto hizo ziweze kupatiwa ufumbuzi wa haraka  na Serikali iweze kushirikiana na sekta binafsi katika miradi mbambali ya kiuchumi na kijamii.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wamechangia juu ya utekelezaji wa mradi wa umwagiliaji kuzorota katika utekelezaji wake hasa kwa upande wa Pemba katika mabonde ya Mlemele na Makwararani licha ya kuwa fedha nyingi zimeshatumika. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara kuzitatua kwa haraka changamoto hizo ili wananchi waanze kunufaika na mradi ule kutokana na kusubiri kwa muda mrefu kwa kutojishughulisha na kilimo cha mpunga katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la upatikanaji na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima nalo limechangiwa na wajumbe wengi, licha ya kuwa Serikali imeshusha bei ya pembejeo kutoka Tzs 50,000 hadi Tzs 10,000 bado pembejeo zimekuwa shida kupatikana. Aidha, wakulima hupata pembejeo kidogo ambazo haziwezi kutosheleza katika mashamba yao hali inayopelekea kupungua kwa uzalishaji wa mpunga na mazao mengine. Hivyo, Serikali inapaswa kujitahidi kutoa pembejeo za kutosha kwa wakulima hao na kuacha kuziweka pembejeo hizo ndani na kutumika katika mwaka mwengine wa bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la bei ndogo ya mwani kwa wakulima nalo limechangiwa na wajumbe wengi na kuonesha kutoridhishwa nayo. **Mheshimiwa Spika,** bei hii ya kilo moja kwa Shilingi 700 bado ni ndogo sana na hailingani kabisa na muda ambao wakulima wanaoutumia katika kushughulikia kilimo hicho. Azma ya Serikali ya awamu ya nane iliyooneshwa na Mhe. Rais alipolihutibia Baraza la Wawakilishi wakati wa ufunguzi wa Baraza la Kumi, alisisitiza sana suala la kuongeza bei ya zao la mwani kwa kufungua viwanda vya kusarifu mwani, kutoa mikopo kwa wakulima wa mwani, kutafuta masoko mapya, ili kuimarisha kipato cha wakulima wa mwani hasa wakina mama. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kutekeleza kwa vitendo azma hii ya Serikali ya awamu ya nane na kulifanya zao la mwani kuwa ni lenye tija kwa wakulima wetu na kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

**Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya wajumbe wamechangia kuhusu Mradi wa Serikali Mtandao (e-Government) nao umechagiwa na wajumbe kwa kutaka kujua utekelezaji wake, kimsingi mradi huu ni muhimu katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Serikali kwa ufanisi mkubwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa kodi kwa njia za kielektroniki. Hivyo, Kamati inaishauri Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Miundombinu kuendeleza mradi huu kwa haraka hususan katika eneo la e-Tax, e-Health na maeneo mengineyo.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini

**Mheshimiwa Spika,** katika wizara hii Wajumbe wengi walichangia katika hoja ya kukosekana kwa huduma ya maji kwa muda mrefu au kutopatikana kabisa kwa huduma hiyo katika baadhi ya maeneo mengi. Kama tujuavyo, maji ni kitu cha lazima, bila ya maji hakuna uhai. Kutokana na umuhimu wake, wananchi wengi hasa kina mama wamekuwa wakitumia muda mkubwa kutafuta maji kiasi ambacho hukosa muda wa kufanya kazi za maendeleo na pia kukosa muda wa kutosha wa kulea watoto wetu kwa ukaribu. **Mheshimiwa Spika,** Wizara hii kupitia ZAWA imekuwa ikitekeleza miradi mingi inayohusiana na upatikanaji wa maji lakini kumekuwa na ufanisi mdogo sana, hivyo tunashauri Serikali ije na mkakati maalum wa kulitatua hili. Ifike mahali, kadhia hii ya kukosekana maji ipunguwe sana au iondoke kabisa.

## HOJA ZA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** Katika bajeti ya mwaka 2021/2022 miongioni mwa changamoto za msingi zilizojitokeza kwa bajeti za wizara tofauti ni pamoja na viashiria vya baadhi ya taasisi kutokuwa na uhalisia pamoja na kutofautiana kasma za fedha baina ya vitabu vya hutuba na vitabu vya Makadirio ya Mapato na Matumizi ambavyo vinatumika katika kupitisha bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Kasoro hii inawezekana ikaonekana kama ni ndogo au ya kawaida sana, lakini katika muktadha wa bajeti hususan kwa bajeti inayoitumia  Programu (Program Based Budget) kuwa na viashiria visivyo

akisi uhalisia maana yake hatuwezi kujipima juu ya malengo na ufanisi wa programu ambazo tunaziidhinishia fedha. Kwa kuwa Serikali imekiri kuwepo kwa kasoro hizo, ni matumaini ya Kamati yangu kuwa kasoro hizo zitachukuliwa uzito mkubwa na Serikali na kufanyiwa kazi ili jambo hili lisijirejee tena katika bajeti zinazofuata miaka ya mbele.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa Bajeti kulijitokeza hoja ya kuwepo kwa utofauti wa takwimu katika baadhi ya vitabu vya Hotuba vinavyowasilishwa na waheshimiwa Mawaziri na Kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Bajeti inayotumia Programu (PBB) hali inayoleta mkanganyiko mkubwa kwa wajumbe. Aidha, katika vitabu vya Hotuba vilivyowasilishwa, kumekosekana taarifa za utekelezaji kwa baadhi ya fedha za Bajeti zilizotengwa na kuwalazimu wajumbe kuomba ufafanuzi zaidi. Hali hii imejitokeza katika fedha zilizotengwa TZS 2.0 bilioni kwa ajili ya utafiti katika bajeti ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe walisisitiza Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kufuatilia na kusimamia kwa karibu Programu ya mafunzo kwa watumishi waliopo kazini na wanaotegemea kustaafu kwani hakuna fungu la pamoja lililotengwa kwa ajili hiyo na badala yake kila taasisi hupangiwa bajeti ya mafunzo kwa watumishi wake. Utaratibu huu sio mzuri kibajeti hasa ikizingatiwa kuwa ipo Wizara maalum iliyopewa jukumu hii.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mjadala wa bajeti, wajumbe walisisitiza umuhimu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Idara yake ya Masuala ya Kodi, kuangalia vyanzo vya mapato vya taasisi mbali mbali za Serikali kwa lengo

la kuvifahamu vyanzo hivyo na hatimae taasisi zinazokusanya kupangiwa makusanyo yenye uhalisia.

**Mheshimiwa Spika,** Eneo jengine ambalo Wajumbe walichangia ni umuhimu wa kuongeza usimamizi wa fedha za miradi ya maendeleo ili kuepusha fedha za miradi kutumika vibaya kinyume na malengo yaliyokusudiwa. Aidha, taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zinazowasilishwa na wakandarasi wanapokuwa katika maeneo ya utekelezaji wa miradi ziende sambamba na taarifa zilizopo katika Wizara husika. Miongoni mwa utofauti wa taarifa umejitokeza katika mradi wa ujenzi wa Skuli ya Kibubwi.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Wakati tukipitisha mafungu ya wizara tofauti Mawaziri wengi wamewaomba Wajumbe kuridhia Bajeti zao zipitishwe kwa msingi kwamba, huu ni mwaka wa mwanzo wa Serikali ya awamu ya nane, hivyo wapewe muda kwenda kuyasimimia mambo ambayo Wajumbe wameyaibua. Kamati inaomba kuwatahadharisha Mawaziri kuhusu ahadi walizozitoa kwa Wajumbe wa Baraza zikafanyiwe kazi ili matokeo yanayotarajiwa kupitia fedha ambazo tunaziidhinisha yaweze kupatikana na hatimae yakawanufaishe wananchi. Kukamilika kwa bajeti ya 2021/2022 iwe ni mwanzo wa matayarisho ya bajeti ya mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba pia kuwakumbusha mawaziri pamoja na watendaji wa Wizara na taasisi zote za Serikali kwamba, bajeti zilizoidhinishwa zinapaswa kutekelezwa kwa kuzingatia malengo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, pamoja na ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwa upande wetu, Wajumbe Baraza la Wawakilishi pia tuna wajibu wa kuisimamia ili kuhakikisha yanayotekelezwa na vyombo vya Serikali yanakwenda sambamba na miongozo ya nyezo hizo muhimu katika utekelelezaji wa bajeti yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia naomba niwaashukuru tena Wajumbe kwa kunistahamilia na kunisikiliza wakati nikiwasilisha hutuba hii ya majumuisho ya mjadala wa bajeti za Wizara zote kwa mwaka 2021/2022.

Ahsanteni na naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Suleiman Ameir

……………………………

Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**